VITABU VYA PROGRAMU YA REDET NA. 16

UWEZEKANO WA KUANZISHA SHIRIKISHO LA AFRIKA MASHARIKI

Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania
(REDET)

Kimechapishwa na
Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania
Idara ya Elimu ya Siasa na Utawala
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35039
DAR ES SALAAM
Tanzania

© **Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania, 2008**
Idara ya Elimu ya Siasa na Utawala
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

ISBN 9987 609 37 6

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutoa au kunakili kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania.

SURA YA NANE

Ongezeko la Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki: Manufaa na Changamoto

Rasul Ahmed & Lupa Ramadhani

Utangulizi

Makala hii inachambua manufaa na changamoto za ongezeko la wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunaweza kuangalia manufaa na changamoto kwa namna tatu tofauti. Kwanza ni manufaa kwa wanachama wapya, pili manufaa kwa wanachama waanzilishi na mwisho manufaa kwa Jumuiya kwa ujumla. Pamoja na hayo kila uamuzi una changamoto na pengine mapungufu yake. Tutajaribu kuainisha changamoto zinazoweza kujitokeza kwa kuongeza wanachama katika Jumuiya. Tumeziita changamoto kwa sababu tunaamini zinaweza ama kufanyiwa kazi na kuboreshwa kadri itakavyofaa kwa wakati husika au zikafumbiwa macho na kuvuruga juhudi za kuungana. Kushamiri na kuimarika kwa shirikisho kutategemea ni kwa kiasi gani changamoto hizi zinaibuka na kushughulikiwa ipasavyo.

Wazo la kutaka kuungana sio geni katika siasa za Afrika. Tangu nyakati za kupigania uhuru viongozi wa Bara la Afrika walikwishaona umuhimu wa kuungana kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Afrika. Waafrika kwa pamoja bila kujali walikuwa Ulaya, Marekani au Afrika walianza kujitambua kuwa kitu kimoja na kuona kuwa silaha yao dhidi ya ugandamizaji ni kuungana. Wakati wa kuunda Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU)

hakukuwa na mjadala juu ya umuhimu wa kuungana. Makundi yote matatu (Casablanca, Monrovia na Brazzaville) yaliyojitokeza yalikubaliana kwa dhati juu ya suala hili. Walitofautiana tu juu ya namna ya kufikia muungano. Tangu wakati huo walikwishaona kuwa isingewezekana kwa bara lililokuwa na watu milioni 230 lenye rasilimali zilizotapakaa lingeweza kuendelea kama lingebaki na vitaifa vidogo karibu 56 (Legum, 1962: 65).

Wale waliotaka muungano ujengwe kuanzia chini kwenda juu (bottom up) walipendelea kuanza na miungano ya kikanda. Jomo Kenyatta alikuwa thabiti kwenye msimamo wake: "...nataka kuiona Afrika Mashariki ikiungana na kisha Afrika yote" (Legum, 1962:65). Hoja ya kambi ya Nyerere inashabihiana na hii. Hoja yake ilikuwa kwamba kwa kuanzia nchi zile ambazo ni majirani na zinafahamiana vizuri zianze kuungana na baadaye ama zivutie nchi nyingine kwenye miungano yao au jumuiya mbalimbali za kikanda zije kuungana baadaye. Nyerere, mathalani, alikwenda mbali zaidi kwa kupendekeza kuwa nchi za Afrika Mashariki zipate uhuru kwa pamoja na ziunde taifa moja. Wasiwasi wake ulikuwa kwamba nchi hizi zikiruhusiwa zipate uhuru moja baada ya nyingine ingekuwa vigumu sana baadaye kuja kuungana. Wazo hili nalo halikuwezekana kutekelezwa. Nkrumah alipinga dhana hii. Alihoji kuwa haja ya kuungana ni muhimu na kubwa kiasi ambacho haiwezi kusubiri nchi kuungana kikanda kwanza. Nkrumah alipendekeza iundwe serikali moja ya Afrika ambayo ingewafanya Waafrika wote kufikiria kama nchi moja. Rais wa Mali, Modeiba Keita, alikwenda mbali zaidi kwa kuweka kipengele kwenye katiba kilichoelezea utayari wa nchi yake kuachia mamlaka ya dola kama nchi nyingine zingekubali kuungana (Legum, 1962: 66). Kwa hiyo jumuiya za kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, ECOWAS, SADC, Umoja wa Bonde la Mto Kagera, pamoja na COMESA huchukuliwa kama hatua kuelekea kwenye Shirikisho kamili la Afrika.

Kinachojidhihirisha ni kwamba kuna faida nyingi za kuungana pengine kuliko za kutengana. Waswahili wana msemo kuwa umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Hii ilijionyesha mara baada ya kusambaratika kwa Shirikisho la Kisoshalisti la Kisovieti la Urusi (USSR) lililokuwa moja ya mataifa makubwa ulimwenguni likishindana na Marekani. Marekani yenyewe ni matokeo ya Muungano wa nchi 50. Sio ajabu kuwa leo

Marekani ni taifa lenye nguvu sana duniani. Wanaotaka kuungana wanadhani wanaweza kufikia mafanikio iliyoyapata Marekani. Hoja ya kukubali wanachama wapya inawezekana ilijikita katika kutambua kuwa kuna manufaa katika ongezeko la wanachama.

Muhtasari wa Hali Ilivyo Ndani ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kabla ya kuzama kwenye mada kuu ya makala hii, si vibaya kama tukitazama, japo kwa muhtasari, taswira ya nchi hizi tano ambazo zimeafikiana kushirikiana kupitia jumuiya ya kikanda ya eneo hili la Afrika Mashariki. Hapa tutawasilisha vielelezo vya kiuchumi, kijamii, kisiasa, na kijiografia. Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa na eneo la ukubwa wa kilomita za mraba milioni 1.85 baada ya kujiunga kwa nchi za Rwanda na Burundi.

Nchi za Rwanda na Burundi ni miongoni mwa nchi 15 zinazoendelea kutoka Afrika ambazo hazina bandari. Idadi ya watu nchini Rwanda inakadiriwa kufikia takriban milioni 8.4 (takwimu za mwaka 2005). Burundi ina idadi ya watu zaidi ya milioni 8.0 (takwimu za 2006). Jumuiya ya Afrika Mashariki inategemewa kukaribia watu milioni 120 baada ya kuongeza uanachama wa nchi za Rwanda na Burundi. Nchi waanzilishi wa Jumuiya, yaani Kenya, Tanzania na Uganda, kwa pamoja zinakadiriwa kuwa na zaidi ya watu milioni 93 (UNCTAD, 2007). Kwa pamoja wanachama wa Jumuiya wanatarajia kuwa na Jumla ya Zao la Taifa la dola za kimarekani milioni 41 (EAC, 2007).

Viwango vya kuzaa vinasemekana kuwa juu zaidi nchini Uganda ambapo kwa wastani mwanamke mmoja anazaa watoto saba, wakati kiwango kiko chini Kenya ambapo kwa wastani mwanamke huzaa watoto wanne (SID, 2006). Kwa viwango hivyo, idadi ya watu nchini Uganda inakadiriwa kufikia takriban milioni 64 ifikapo mwaka 2030, ambapo nchi hiyo itakuwa inaongoza kwa idadi ya watu katika ukanda huu ikifuatiwa na Tanzania (milioni 57), Kenya (milioni 41) na Rwanda (milioni 13.4). Afrika Mashariki pia kwa sasa inashuhudia ukuaji wa haraka wa miji ingawa idadi kubwa ya wakazi wa mijini wanaishi kwenye makazi duni na yasiyopimwa.

Ukanda wa Afrika Mashariki unategemea nishati ya umeme kutoka

vyanzo vya maji. Ingawa mahitaji ya nishati hiyo ni makubwa uzalishaji ni chini ya asilimia ishirini ya idadi ya watu wa ukanda mzima.

Hali ya maisha ya watu katika nchi wanachama wapya wa Jumuiya iko chini ya ile ya wanachama wengine. Kwa mujibu wa moja ya Ripoti za Shirika la Fedha Duniani (IMF) kuhusu Rwanda, nchi hiyo pamoja na kutimiza malengo matatu ya Milenia (MDGs) katika maeneo ya chanjo, kupunguza maambukizo ya UKIMWI, na kuondoa tofauti za jinsia katika elimu ya msingi, Benki ya Dunia inaamini kuwa ili nchi hiyo iweze kutimiza malengo mengine ya Milenia, itahitajika misaada zaidi ya fedha. Kwa sasa Benki hiyo inaona ni vigumu kabisa kutimiza baadhi ya malengo, hususan kupunguza idadi ya watu wanaoishi kwa gharama ya chini ya dola moja ya Kimarekani kwa siku. Sekta ya kilimo inaajiri zaidi ya asilimia tisini ya wakazi wa nchi za Jumuiya na sekta isiyo rasmi inaelekea kuwa chanzo muhimu cha ajira katika nchi za Kenya, Tanzania na Uganda, ukuaji wa sekta hii ukiendana na kupanuka kwa miji mikubwa katika nchi hizo.

Umaskini na tofauti kubwa ya kipato katika nchi za Afrika Mashariki bado ni changamoto kubwa inayokabili ukanda huu. Magonjwa ya UKIMWI, Malaria na Kifua kikuu yanachangia kwa kiwango kikubwa kushusha umri wa kuishi wa wakazi wa eneo hili. Wastani wa viwango vya wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano wanaofariki bado viko juu kuliko maeneo mengine Kusini mwa Sahara.

Nchi za Rwanda na Burundi zinategemea sana sekta ya mawasiliano ya nchi waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mradi mkubwa wa kuimarisha mawasiliano ya barabara unaosimamiwa na Jumuiya kwa ushirikiano na wafadhili unatarajiwa kuzinufaisha nchi wanachama, hususan Rwanda na Burundi katika kuagiza na kusafirisha bidhaa zao. Rwanda, kwa mfano, haina kiunganishi cha reli kufikia Tanzania ingawa mawasiliano ya karibu ya reli toka mji wa Kigali ni Kilomita 380 mpaka mji wa Isaka, Tanzania. Mawasiliano kwa njia ya reli kwa upande wa Tanzania yanachukua takriban kilomita 3,500. Shirika la Reli la Tanzania (TRC) lina njia kuu mbili zenye kuchukua umbali wa kilomita 2,600. Reli ya kati kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora (850 km), Tabora mpaka Kigoma (453km) na njia nyingine mpaka Mwanza (386km); na pia reli ya kaskazini kuanzia Tanga na kupitia Moshi mpaka Arusha (430 km). Reli ya TAZARA ambayo inamilikiwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Zambia ina njia ya

urefu wa kilomita 1,860, kilomita 900 kati ya hizo zikiwa ndani ya Tanzania. Reli ya TAZARA inaunganisha Jiji la Dar es Salaam na mji wa Kapiri Mposhi ulioko Zambia.

Shirika la Reli la Kenya (KRC) linatumia njia ya urefu wa kilomita 2,700 inayounganisha Mombasa na mji wa mpakani wa Tororo nchini Uganda. Kwa upande wake Shirika la Reli la Uganda (URC) lina njia ya urefu wa kilomita 1,300 ikiunganisha Kampala na mji wa Malaba uliopo mashariki na Kasese uliopo magharibi mwa nchi hiyo, na kuunganisha miji ya Tororo na Pakwach kaskazini mwa Uganda. Hivi sasa mashirika haya ya reli yako katika zoezi la kubinafsishwa. Katika miaka ya hivi karibuni nchi waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikuwa wanafikiria kuunda shirika moja la reli la muunganiko kwa makubaliano maalum. Hata hivyo mwaka 2003 Tanzania ilijitoa kwenye mazungumzo hayo. Mwaka uliofuata Serikali za Kenya na Uganda ziliamua kusaini Mkataba wa Maridhiano ya kumilikisha kwa pamoja mashirika ya KRC na URC kwa kipindi cha miaka 25.

Mnamo mwaka 1998 Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ilibainisha barabara kuu tano zenye kuunganisha miji mbalimbali ya mipakani ya nchi za Kenya, Tanzania na Uganda. Barabara hizo kwa ujumla zina urefu wa kilomita 15,273. Barabara hizo ambazo zinajulikana kama Regional Corridors ni:

1. Mombasa-Malaba-Katuna (Kenya & Uganda);
2. Dar es Salaam-Mutukula-Masaka (Tanzania & Uganda);
3. Biharamulo-Mwanza-Sirari-Lokichogio (Tanzania & Kenya);
4. Tunduma-Mbeya-Arusha-Isiolo-Moyale (Tanzania & Kenya); na
5. Nyakanazi-Kasulu-Tunduma (Tanzania)

Barabara hizi ni takriban asilimia nane ya jumla ya barabara zilizopo kwenye nchi tatu za Jumuiya, na ni asilimia 42 tu zenye viwango vya lami (SID, 2006: 46). Afrika Mashariki inahudumiwa na bandari sita zilizopo Bahari ya Hindi: Dar es Salaam, Mombasa, Tanga, Zanzibar, Pemba na Mtwara.

Kwa upande wa mifumo ya siasa na utawala nchi wanachama wa Jumuiya zinafanana kwenye masuala kadhaa. Mathalani, nchi zote ni Jamhuri za kikatiba (constitutional republics) zenye vyombo vya kutunga sheria vinavyochaguliwa kupitia chaguzi zenye kushirikisha vyama vingi

kwa vipindi maalum. Nchi zote zinaongozwa na marais wanaochaguliwa na wapiga kura wenye sifa za kupiga kura kwa mujibu wa sheria za uchaguzi za nchi husika kushika hatamu za uongozi kwa kipindi cha miaka mitano, isipokuwa Rwanda ambapo Rais amepewa kipindi cha miaka saba. Ukiondoa Uganda ambapo hakuna kikomo kwa muhula wa Urais, nchi nyingine zote za Jumuiya zinaruhusu vipindi viwili tu vya Urais. Jedwali lifuatalo linatoa muhtasari wa mifumo ya kiutawala ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki:

Jedwali Na 1: *Miundo ya Kiutawala*

	TANZANIA	KENYA	UGANDA	RWANDA	BURUNDI
Uhuru	9. 12.1961	12.12.1963	9.10.1962	1.7.1962	1.7.1962
Muundo wa dola	Jamhuri ya Muungano	Jamhuri	Jamhuri	Jamhuri	Jamhuri
Mgawanyo wa kiutawala	Mikoa 26	Majimbo 8	Wilaya 56	Majimbo 12	Majimbo 17
Uchaguzi wa mwisho	Desemba 2005	Desemba 2002	Februari 2006	Agosti 2003	Julai 2005
Mkuu wa nchi	Rais: Utawala miaka 5	Rais: Utawala miaka 5	Rais: Utawala: Hakuna ukomo	Rais: Utawala miaka 7	Rais: Utawala miaka 5
Safu ya uongozi	Rais: Jakaya Mrisho Kikwete Makamu wa Rais: Ali Mohamed Shein Waziri Mkuu: Edward Lowassa Rais wa Zanzibar: Amani Abeid Karume	Rais: Mwai Kibaki Makamu wa Rais: Moody Awori	Rais: Yoweri Museveni Waziri Mkuu: Apollo Nsibambi	Rais: Paul Kagame Waziri Mkuu: Bernard Makuza	Rais: Pierre Nkurunzinza Makamu wa Rais: Martin Ndiwumana Gabriel Ntisezerana
Bunge	Chemba 1 Wabunge 323 232 wa kuchaguliwa	Chemba 1 Wabunge 224 210 wa kuchaguliwa	Chemba 1 wabunge 305 214 wa kuchaguliwa	Chemba 2 wabunge 80 50 wa kuchaguliwa. Senti wajumbe 24	Chemba 2 wabunge 118 seneti wajumbe 49
Lugha	Kiswahili; Kiingereza	Kiswahili, Kiingereza	Kiswahili, Kiingereza	Kifaransa, Kiingereza, Kinyarwanda	Kifaransa, Kirundi, Kiswahili

Vyanzo: *SID, Tovuti za Taifa za nchi husika.*

Katika masuala ya ulinzi na usalama, tukinukuu ripoti ya taasisi isiyo ya kiserikali yenye matawi katika nchi 125 duniani, iitwayo The Society for International Development (SID) ukanda wa Afrika Mashariki umeshuhudia

jumla ya migogoro (yenye vurugu na isiyo na vurugu) ishirini na saba kati ya mwaka 1952 na 2004. Ripoti hiyo iliyochapishwa mwaka 2006 inaeleza kuwa mwaka 2004 ukanda huu ulihifadhi wakimbizi wapatao milioni 1.14. Tanzania pekee ilikuwa na wakimbizi 602,000, asilimia 74 wakitokea Burundi; na asilimia 26 kutoka DR Congo. Uganda ilipata wakimbizi wapatao 250,000; asilimia 86 wakitokea Sudan, asilimia 7.5 kutoa Rwanda na asilimia 6 kutoka DR Congo. Kenya ilihifadhi wakimbizi 239,285 kutoka Somalia (64%), Sudan (28%), na Ethiopia (5.2%). Rwanda nayo ikiwa na asilimia 91 (50,221) ya wakimbizi toka DR Congo. Nchi hizo pia zimekuwa zikishiriki kutoa wanajeshi katika shughuli za kulinda amani katika sehemu mbalimbali. Katika kipindi kati ya mwaka 1997 na 2004 ukanda wa Afrika Mashariki ulichangia katika shughuli za kulinda amani mara 97. Kenya ikiongoza kwa kutuma majeshi mara 64, ikifuatiwa na Tanzania (15), Rwanda (8) na Uganda (5) (SID, 2006). Tanzania imepeleka wanajeshi wake kwenye vikosi vya Umoja wa Mataifa nchini Lebanon, Rwanda inashiriki kwenye vikosi vya Umoja wa Afrika (AU) vilivyoko Sudan, na Uganda imepeleka wanajeshi wake Somalia. Kwa muda mrefu vikosi vya Afrika Kusini vimekuwa vikisaidia kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya amani nchini Burundi.

Nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki zina uanachama kwenye jumuiya nyingine za kikanda na mashirika ya kimataifa baadhi yakiwa na malengo yanayokaribiana kabisa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jedwali lifuatalo linaonyesha uanachama wa nchi zinazounda Jumuiya katika jumiya nyingine za kikanda.

Jedwali Na 2: *Ushiriki wa Wanachama Kwenye Jumuiya Nyingine za Kikanda*

	KENYA	TANZANIA	UGANDA	RWANDA	BURUNDI
COMESA	√	×	√	√	√
SADC	×	√	×	×	×
IGAD	√	×	√	×	×
CBI	√	√	√	√	√
IOC	√	√	×	×	×
NILE BASIN	√	√	√	√	√
EAC	√	√	√	√	√
AU	√	√	√	√	√

Ongezeko la Wanachama wa Jumuiya za Kikanda: Tafakuri za Kinadharia na Tunayojifunza Kutoka Jumuiya ya Ulaya (EU)

Tafakuri za Kinadharia

Kinadharia, mada ya kutanuka wigo wa jumuiya za kikanda lilianza kuvutia wasomi tangu pale Jumuiya ya Ulaya (EU) ilipopata ongezeko la kwanza la wanachama (Denmark, Uingereza na Ireland). Ilipotokea ongezeko la pili (Ugiriki) na la tatu (Hispania na Ureno) mjadala ulishapata wachangiaji wengi. Wachambuzi wengi wa mjadala huu wamekuwa wakijadili kwa kuangalia maeneo tofauti kama vile: athari za ongezeko kwa jumuiya yenyewe, wanachama wapya na wa zamani; mwingiliano wa tamaduni; vigezo vya kuruhusu wanachama wapya; sababu zinazosukuma nchi kujiunga na jumuiya, na kadhalika. Ni vigumu kwetu kuitendea haki vilivyo sehemu hii kwa kuwa hatutaweza kurejea mitazamo yote ya wachambuzi wa mjadala huu. Lakini si vibaya tukirejea japo mawazo ya wachambuzi wachache.

Wanazuoni wameandika sana kuhusu dhana nzima ya nchi kuungana. Baadhi ya wanazuoni wanaamini kuwa kinachowaunganisha watu kwa pamoja ni ubinadamu wao. Kwa pamoja binadamu wote wana mahitaji (needs) yanayolingana bila kujali mipaka ya nchi. Wanaona kuwa wakati mahitaji ya binadamu huwaleta watu pamoja, siasa huwatenganisha watu. Kwa mfano wakati wa mafuriko yaliyotokea kule New Orleans, Marekani, ilibidi nchi ipokee misaada bila kujali inatoka wapi. Kwa wakati ule kilichowasukuma mataifa mengine kutoa misaada ilikuwa ubinadamu. Kwamba binadamu anahitaji mahali pazuri pa kulala na kwamba hapati maradhi yatakayotishia afya yake. Ugonjwa kama polio hauheshimu mipaka ya nchi na ulipolipuka ililazimu nchi kufanya juhudi za pamoja kuutokomeza maana isingefaa kitu kama nchi moja pekee yake ingeanzisha kampeni ya kupambana na polio bila kuzishirikisha nyingine. Polio ingepenya na kurudi katika nchi ile na wananchi wangeteketea. Hii pia ni kweli kwa ugonjwa kama UKIMWI. Hivi sasa dunia imeshuhudia matatizo ya kimataifa. Ugaidi, biashara ya fedha haramu, biashara ya madawa ya kulevya hufanyika bila kuangalia mipaka ya nchi na yana athari kwa dunia nzima kwa ujumla.

Wakati hali ikiwa hivi, nchi zinajiona kuwa na wajibu wa kwanza wa kutimiza mahitaji ya wananchi wake. Ukweli, hata ni kuwa uwezo wa nchi mojamoja kutimiza mahitaji hayo unapungua na hivyo kufanya umuhimu wa kuungana kuwa mkubwa. Ukweli huu pengine ni vigumu kukubalika kwa kuwa nchi nyingi hazipendi kupoteza mamlaka yao ya kidola. Kazi kubwa imekuwa katika kutafuta uwiano kati ya siasa na mahitaji.

Wanazuoni wengine wamejikita katika kuangalia kwa nini jumuiya za kikanda huanzishwa na kudumu au kudhoofika na kufa kabisa. Hawa wamefanya tathmini ya viungo muhimu vya kutengeza jumuiya hizi. Jumuiya za kikanda zinaweza kuundwa na kudumu ikiwa tu baadhi ya mambo yatazingatiwa. Katika modeli yake ya hivi karibuni, Baregu (2007) anaelezea misingi mikuu minne ya kuungana kwamba nchi zinazoungana lazima zipendane, zione manufaa ya kuungana, kuwe na tishio na mamlaka. Baregu anaendelea kuelezea kuwa misingi hii inaweza ikaja ama kwa hiari au kwa uhitaji. Isitoshe Baregu anaainisha kuwa kwa kadri ambavyo uhitaji unaongezeka ndivyo ambavyo hiari inatoweka. Anasema kuwa hufikia mahali suala la kuungana huwa ni la uhitaji na sio hiari. Baregu anaiona Jumuiya ya Afrika Mashariki kama iliyoegemea zaidi kwenye mapenzi na manufaa. Anatolea mfano wa Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao unaelezea kuwa nchi za Afrika Mashariki zina uhusiano wa kihistoria wa kibiashara, kiuchumi, kitamaduni n.k. Mkataba unaelezea pia manufaa ya kuungana kuwa ni mgawanyo ulio sawa wa mapato ya Jumuiya. Baregu anaamini kuwa kwa kuangalia uchumi wa nchi hizi na uwezekano wa kushindana katika dunia ya utandawazi, Shirikisho la Afrika Mashariki ni suala la uhitaji na sio hiari.

Mattli (1999) amekuwa mashuhuri katika uchambuzi wa masuala ya Jumuiya za kikanda. Amefanya uchambuzi wa Jumuiya za kikanda zilizowahi kuundwa hasa akilenga kuangalia msukumo wa kuanzishwa kwake. Akiangalia hoja ya ongezeko la wanachama, Mattli anasema kuwa nchi ambazo zipo nje ya jumuiya zikipata athari yoyote (hasi au chanya) ya kuwepo kwa jumuiya hiyo zaweza kuchukua moja ya hatua zifuatazo: kwanza zinaweza kuamua kujiunga na jumuiya hiyo, pili zinaweza kuamua kuunda jumuiya nyingine tofauti na hiyo. Mwitikio wa kwanza (yaani kujiunga na jumuiya) unawezekana tu kama nchi wanachama wa Jumuiya wako tayari kukubali wanachama wapya. Kama wanachama wanaona

nchi inayoomba uanachama haiwezi kuleta faida kwenye Jumuiya zinaweza kuikataa na hivyo nchi hiyo kulazimika kuangalia uwezekano wa mwitikio wa pili, yaani kuunda Jumuiya mpya.

Kundi lingine la wanazuoni hujulikana kama Wanashirikisho kwa ujumla wao. Kundi hili linahusisha wasomi kama David Mitrany ambao wanaamini kuwa ili kuwa na Shirikisho ni lazima nchi zikubali kuachia madaraka fulani ya dola. Wanaelewa kuwa ni vigumu sana kwa dola kukubali kuachia madaraka lakini kwa kadri ambavyo dola inalazimika kushirikiana na nchi nyingine, taratibu dola inaanza kupoteza baadhi ya udhibiti wake. Hawa wanaamini katika kazi za dola. Wao wanaamini kuwa kuna kazi ambazo ili zifanyike kwa ufanisi ni lazima ziwe katika kiwango cha kimataifa zikishirikisha nchi kadhaa. Mfano tulioutoa hapo juu kuhusu polio, UKIMWI na uhalifu wa kimataifa ni mojawapo ya shughuli ambazo nchi lazima zishirikiane ili kupata ufanisi. Wanasema pamoja na kuwa inaonekana kuwa ushirikiano wa aina hii sio tishio kubwa kwa mamlaka ya dola, lakini taratibu uhusiano huu hugusa siasa za mkondo mkuu (high politics) (Brown, 2001: 132). Wanatolea mfano Umoja wa Ulaya ambao ulianza na Jumuiya ya Makaa ya Mawe na Chuma (Siasa za mkondo mdogo) lakini taratibu ikaanza kwenda kwenye mkondo mkuu ilipoundwa Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya na sasa ambapo nchi zinafikiria kuanzisha shirikisho, ambapo kimsingi nchi mojamoja zitapoteza mamlaka karibu yote ya dola na kuyahamishia katika Umoja wa Ulaya. Mpaka sasa kuna sera ya pamoja ya nje, sarafu moja na benki kuu yake ambayo inajumuisha nchi 12. Haya ni mamlaka ambayo nchi haikubali kuyapoteza kirahisi, isipokuwa tu ikidhihirika kuwa ni njia pekee ya kujiimarisha katika siasa za kimataifa.

Akichambua matarajio ya ushirikiano wa kiuchumi, Thomas Straubhaar (2002) anafananisha suala la uraia wa taifa na uanachama wa klabu. Anasema kwenye klabu nyingi wanachama wa siku nyingi huwa tayari kuwapokea wanachama wapya, na kuifanyia marekebisho klabu kuendana na dunia ya nje. Straubhaar anaendelea kusema kuwa marekebisho hayo ndiyo yanayoihakikishia klabu kuendelea kuwepo. Lakini kama klabu itaongezeka ukubwa haraka sana, wanachama wake watakosa kujiamini na kuona uanachama na utambulisho wao uko mashakani na hali hiyo ikitokea inaweza kuwafanya wageukie vitendo vya kujihami. Vivyo hivyo kwa ushirikiano wa kikanda, siasa za ndani za nchi wanachama zina nafasi kubwa katika kushawishi watu waikubali jumuiya na waone masuala ya

nchi inayoomba uanachama haiwezi kuleta faida kwenye Jumuiya zinaweza kuikataa na hivyo nchi hiyo kulazimika kuangalia uwezekano wa mwitikio wa pili, yaani kuunda Jumuiya mpya.

Kundi lingine la wanazuoni hujulikana kama Wanashirikisho kwa ujumla wao. Kundi hili linahusisha wasomi kama David Mitrany ambao wanaamini kuwa ili kuwa na Shirikisho ni lazima nchi zikubali kuachia madaraka fulani ya dola. Wanaelewa kuwa ni vigumu sana kwa dola kukubali kuachia madaraka lakini kwa kadri ambavyo dola inalazimika kushirikiana na nchi nyingine, taratibu dola inaanza kupoteza baadhi ya udhibiti wake. Hawa wanaamini katika kazi za dola. Wao wanaamini kuwa kuna kazi ambazo ili zifanyike kwa ufanisi ni lazima ziwe katika kiwango cha kimataifa zikishirikisha nchi kadhaa. Mfano tulioutoa hapo juu kuhusu polio, UKIMWI na uhalifu wa kimataifa ni mojawapo ya shughuli ambazo nchi lazima zishirikiane ili kupata ufanisi. Wanasema pamoja na kuwa inaonekana kuwa ushirikiano wa aina hii sio tishio kubwa kwa mamlaka ya dola, lakini taratibu uhusiano huu hugusa siasa za mkondo mkuu (high politics) (Brown, 2001: 132). Wanatolea mfano Umoja wa Ulaya ambao ulianza na Jumuiya ya Makaa ya Mawe na Chuma (Siasa za mkondo mdogo) lakini taratibu ikaanza kwenda kwenye mkondo mkuu ilipoundwa Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya na sasa ambapo nchi zinafikiria kuanzisha shirikisho, ambapo kimsingi nchi mojamoja zitapoteza mamlaka karibu yote ya dola na kuyahamishia katika Umoja wa Ulaya. Mpaka sasa kuna sera ya pamoja ya nje, sarafu moja na benki kuu yake ambayo inajumuisha nchi 12. Haya ni mamlaka ambayo nchi haikubali kuyapoteza kirahisi, isipokuwa tu ikidhihirika kuwa ni njia pekee ya kujiimarisha katika siasa za kimataifa.

Akichambua matarajio ya ushirikiano wa kiuchumi, Thomas Straubhaar (2002) anafananisha suala la uraia wa taifa na uanachama wa klabu. Anasema kwenye klabu nyingi wanachama wa siku nyingi huwa tayari kuwapokea wanachama wapya, na kuifanyia marekebisho klabu kuendana na dunia ya nje. Straubhaar anaendelea kusema kuwa marekebisho hayo ndiyo yanayoihakikishia klabu kuendelea kuwepo. Lakini kama klabu itaongezeka ukubwa haraka sana, wanachama wake watakosa kujiamini na kuona uanachama na utambulisho wao uko mashakani na hali hiyo ikitokea inaweza kuwafanya wageukie vitendo vya kujihami. Vivyo hivyo kwa ushirikiano wa kikanda, siasa za ndani za nchi wanachama zina nafasi kubwa katika kushawishi watu waikubali jumuiya na waone masuala ya

tamaduni nyingine kama fursa. Kama hilo litashindikana hata ushirikiano wa kiuchumi wenye mafanikio unakuwa hatarini kuporomoka. Shams (2002) yeye anaona ongezeko la wanachama linavumbua matatizo mapya lakini linazuia muungano kuonekana kama umefungwa kwa wengine kujiunga. Kwa upande wake, Wangwe (2002: 179) akisadifu uwezo mdogo wa sekta ya uzalishaji wa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki anadhani jumuiya hiyo lazima ielekeze nguvu za kuongeza uwezo wa kuzalisha bidhaa na kutoa huduma na kuongeza kiwango cha ushindani. Anapendekeza kuwa inafaa kwa Jumuiya hiyo kuwa na "Mwegemeo wa Maendeleo" kuliko "Mwegemeo wa Soko" ambao Wangwe anabainisha kuwa umekosolewa na wasomi kama Gunnar Myrdal kwa athari zake.

Tukimrejea Shams (2002), yeye anaona jambo moja la kujifunza toka Umoja wa Ulaya ni kwamba haukusukumwa tu kuwepo na tathmini ya gharama na manufaa ya kiuchumi, bali ni dira kuu ya amani na usalama wa Ulaya. Ushirikiano wa kiuchumi ukatumika kama njia ya kufikia ushirikiano wa kisiasa. Katika makala za wachambuzi kadhaa wanaoangalia kukua kwa Umoja wa Ulaya, misamiati wa "Europeanization" na "Eastward enlargement" inatumika sana haswa baada ya nchi nyingi za Ulaya Mashariki kujiunga na umoja huo. Kwenye ukanda wetu kwa sasa tunaweza kusema kilichotokea ni "Westward enlargement" na si ajabu kabisa siku za usoni wachambuzi wetu wakatumia msamiati wa "Eastafricanization" pale wakazi wa wanachama wapya wa jumuiya watakapokuwa wanaiga tamaduni na stadi za maisha za wanajumuiya wanzilishi. Kinadharia, pia kama Jumuiya ya sasa itafanikiwa kuwa kubwa, yenye nguvu kiuchumi na sauti kisiasa, twaweza siku zijazo tukajadili hoja ya "Pax-EastAfricana!"

Tunayojifunza Kutoka Umoja wa Ulaya

Ni vizuri kuangalia Umoja wa Ulaya ili kupata uzoefu unaoweza kuwa wa manufaa kwa ukanda wetu wa Afrika Mashariki. Umoja wa Ulaya ni kati ya Jumuiya chache za kikanda ambayo imepata mafanikio makubwa. Jumuiya hii iliyoanzishwa kama ushirikiano wa kiuchumi ikihusisha nchi sita tu mwaka 1952 imeendelea kukua sio tu kwa kuweza kuvutia wanachama wapya, bali pia kwa kuimarisha ushirikiano mpaka kufikia

kufikiria kuwa na shirikisho. Kufikia mwaka 2007 Umoja wa Ulaya una nchi wanachama 27 na bado maombi ya uanachama ya nchi nyingine yanaendelea kupokelewa. Kwa kiasi fulani Jumuiya ya Afrika Mashariki ilionekana kufuata mkondo wa Jumuiya ya Ulaya. Ushirikiano ulianza katika maeneo machache ambayo hayaonekani kugusa mkondo mkuu wa siasa (ukihusisha hasa masuala ya kiuchumi na kijamii). Hata hivyo wakati Umoja wa Ulaya ulichukua miaka mingi na kujengeka taratibu, Jumuiya ya Afrika Mashariki inaonekana kutotaka kusubiri na kujaribu kuharakisha baadhi ya hatua. Lakini muhimu kwa makala yetu ni kutaka kujua namna ambavyo wanachama wapya waliingizwa kwenye Jumuiya na kuona kama ongezeko hili la wanachama litakuwa na tija iliyokusudiwa. Tutaanza kwa kuelezea historia ya upanukaji wa Umoja wa Ulaya.

Umoja wa Ulaya ulianza mwaka 1952 ukihusisha nchi sita zilizoanzisha Jumuiya ya Makaa ya Mawe na Chuma. Nchi hizo ni Ubelgiji, Uholanzi, Luxembourg, Ufaransa, Italia na Ujerumani Magharibi. Tangu kuanzishwa kwake wanachama wapya wamekwishaongezwa mara tano. Ongezeko kubwa kabisa la wanachama kuwahi kufanywa kwa mara moja ni ongezeko la tano lililofanywa tarehe 1 Mei 2004, wakati ambapo nchi 8 zilijiunga kama awamu ya kwanza. Awamu ya pili ziliingiwa Bulgaria na Romania tarehe 1 Januari 2007 hivyo kufanya idadi ya nchi 10 kuongezwa kwa mkupuo. Itakumbukwa kuwa katika Umoja wa Ulaya, nchi hizi sita waanzilishi zimeendelea kubaki kuwa vinara wa Umoja na kwa kiasi kikubwa kutoa mwongozo na mwelekeo kwa nchi nyingine. Wakati ambapo nchi nyingine zilisita kuingia katika umoja wa sarafu, nchi hizi zote ni wanachama wa umoja huo. Wakati huohuo Ujerumani imeonekana kama ndio injini ya Umoja wa Ulaya. Inategemewa kutoa uongozi wa jumla kwa nchi nyingine, na hata kubeba gharama za kuungana.

Mchakato mzima wa kuongeza wanachama hujulikana kama "European integration"au uunganishaji wa Ulaya. Hii ni kwa sababu mchakato huu huhusisha utaratibu ambapo nchi polepole huachia baadhi ya mamlaka kwa asasi za kikanda za Ulaya. Ili kujiunga na Umoja wa Ulaya, nchi inabidi itimize masharti ya kisiasa na kiuchumi yanayojulikana kama "Vigezo vya Coppenhagen" kufuatia mkutano wa Coppenhagen wa mwaka 1993.

Kwa ujumla kulingana na vigezo vya Coppenhagen ili nchi ifikiriwe kuwa mwanachama wa Umoja wa Ulaya inabidi iwe ni nchi inayoongozwa na sheria za kisekula (sio ya kidini); iwe na serikali ya kidemokrasia, iwe na utawala wa kisheria na iruhusu uhuru na haki za binadamu. Kwa mujibu wa Mkataba wa EU ili nchi kupewa uanachama, inatakiwa ikubaliwe na nchi wanachama wa sasa pamoja na Bunge.

Ili kuwa mwanachama, nchi hupitia mchakato mrefu ikiwa ni pamoja na kurekebisha uchumi wake ili kuendana na hali ya kiuchumi ya nchi wanachama. Hata hivyo uzuri ni kuwa Umoja wa Ulaya umeweka utaratibu maalum wa kuzisaidia kiuchumi nchi zinazoomba uanachama ili ziweze kuboresha uchumi wao kufikia viwango vilivyokubaliwa. Mpango huu hujulikana kama "the European Community's Phare program" ulioanzishwa mwaka 1989. Masharti mengine ambayo inabidi yatimizwe kabla ya nchi kukubaliwa ni pamoja na:

1. Uthabiti wa taasisi zinazolinda demokrasia, utawala wa sheria, haki za binadamu na haki za makundi maalum;

2. Kuwepo kwa soko huria na uwezo wa kupambana na ushindani wa soko la Ulaya; na

3. Uwezo wa kufuata masharti ya uanachama ikiwemo kuheshimu malengo ya kuungana ya kiuchumi, kisiasa na kisarafu.

Akielezea manufaa ya kuongeza wanachama wapya Liinekanen (2004), Kamishna wa Tume ya Ulaya ya Biashara na Jamii Habari, alisema kuwa nchi 10 zilizoongezwa zimekuja na watu milioni 75 zaidi kwenye Jumuiya. Wameleta utamaduni mpya, historia mpya na uzoefu na maarifa ambayo yataifaa Jumuiya kwa ujumla. Baadhi ya nchi zilizopewa uanachama zina pato la taifa na mitaji mikubwa zaidi kuliko hata baadhi ya wanachama wa EU. Kwa hiyo alisema hatua hii imekuwa na manufaa kwa pande zote mbili kwani sasa nchi hizi zinapata fursa nzuri zaidi ya kulitumia soko la Ulaya, biashara imekuwa wazi zaidi na ubadilishanaji wa fedha umerahisishwa. Nchi zimeweza kutumia teknolojia nzuri zaidi katika uzalishaji.

Faida nyingine ni kwa makampuni yaliyopo kwenye nchi wanachama wa awali wa Umoja wa Ulaya. Haya yanafaidika kwa sababu nchi zilizojiunga zinalazimika kununua na kuwekeza katika teknolojia mpya ili kuendana na masharti ya Umoja wa Ulaya hasa kuhusiana na usalama mahali pa kazi na mazingira. Kwa mfano, biashara katika vifaa vya usalama na mazingira imeongezeka kwa asilimia 5 ikilinganishwa na kabla ya kuingia kwa nchi nyingi kwenye Umoja wa Ulaya. Pia kulikuwa na matumaini kuwa makampuni yataweza kuungana na hivyo kuongeza nguvu zao za uzalishaji na ushindani (Liinekanen, 2004).

Hata hivyo kikwazo kikubwa kilikuwa tofauti za kiuchumi. Pato kwa kichwa lilikuwa chini kwa asilimia 60 ya viwango vya Ulaya. Hali ilitofautiana kati ya asilimia 70 chini ya wastani huko Latvia mpaka asilimia 31 huko Slovenia. Kwa ajili hii wachumi wanakadiria kuwa kwa kasi hii itazichukua nchi zilizojiunga kati ya miaka 15 mpaka 40 kuzifikia nchi za Umoja wa Ulaya. Hali hata hivyo, inatofautiana kutoka nchi moja mpaka nyingine kwani nchi zilizoendelea zaidi kama vile Jamhuri ya Czech, Estonia, Hungary na Slovakia sasa zinafanya biashara kubwa ya kuuza teknolojia yao kwa nchi nyingine za Umoja wa Ulaya. Nchi hizi hufanya biashara ya teknolojia ya viwanda yenye ukubwa sawa tu na Uingereza na Ireland. Nchi hizi zinaonekana kutumia viwanda ambavyo hutumia mitambo zaidi kuliko nguvukazi (labour intensive). Katika nchi ambazo hazijaendelea vizuri kama vile Latvia na Lithuania, kiwango kikubwa cha biashara ya nje huzalishwa kwa kutumia viwanda vinavyotegemea nguvu kazi.

Lakini inasemekana kuwa wanachama wapya wanafaidika kwa kuwa sasa wajasiriamali wa Ulaya hupeleka vitega uchumi vyao katika nchi mpya zilizojiunga kwa sababu gharama za uzalishaji na hasa mishahara bado ipo chini katika nchi hizi. Inakadiriwa, kwa mfano kuwa nchini Hungary asilimia 70 ya mauzo ya bidhaa za viwandani yanatokana na uzalishaji kutoka katika makampuni ya kutoka Ulaya yaliyowekeza. Nchi hizi pia zimeweza kuvutia viwanda vingi vya nguo. Faida kubwa inayoonekana ni kuwa badala ya kupeleka mitaji hii,,ambayo pia ni ajira, katika mataifa ya Asia, mitaji hii imeweza kubaki Ulaya. Nchi wanachama wapya hivyo wananufaika kiasi fulani kwa teknolojia inayopelekwa huko na wajasiriamali wakati nchi wanachama wa zamani zinafaidika kwa kupunguza gharama za uzalishaji.

Katika makala yake, Raimo (2006: 132) anagusia kuwa kwa kujiunga na Umoja wa Ulaya nchi wanachama zilifanya mageuzi makubwa ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kisheria. Anasema kwa ujumla demokrasia imeimarika zaidi, maelewano kati ya tamaduni tofauti yameimarika, haki za binadamu zinaheshimiwa zaidi na umiliki binafsi (private property) umekuwa nguzo ya uchumi. Lakini pia anaongeza kuwa kwa kujiunga na Umoja wa Ulaya nchi hizi zimeweza kujiunga na jumuiya nyingine za kimataifa na kunyumbulisha sera zao za nje ili ziendane na nchi waanzilishi wa Umoja wa Ulaya.

Akiandika kuhusu changamoto zinazoukabili Umoja wa Ulaya Burgio (2006:96) anaainisha kuwa tatizo kubwa ni kuwa upanuzi wa Umoja wa Ulaya hauonekani kwenda sambamba na uimarishaji wa Umoja. Changamoto inayojitokeza ni kuwa pamoja na kuwa kuna uimarishaji mkubwa wa muungano kwa upande wa uchumi, bado hakujawa na uimarishaji wa kutosha kisiasa. Anagusia kuwa kwa kukosa utashi wa kisiasa wa kutosha inaonekana katiba ya sasa ya Umoja wa Ulaya haiwezi kukabiliana na tofauti za kijamii na kikanda kadri umoja unavyotanuka. Ni katika hali hii ya kutokuiamini Katiba ya Umoja wa Ulaya (the Constitutional Treaty) ndio sababu Katiba ilipigiwa kura ya 'Hapana' na Ufaransa na Ujerumani mwaka 2005 kufuatia kura ya maoni katika nchi hizo. Matokeo ya kura hizi yalizifanya nchi nyingine zilizotaka kuendesha kura ya maoni ama kuahirisha zoezi hilo au kufikiria kutafuta utaratibu mbadala wa kupata maoni. Nchi kama Uingereza, Sweden, Denmark, Czech Republic na Poland zilihofia kura ya Hapana na hivyo kuahirisha zoezi la kukusanya kura za maoni. Wakati wananchi wanaonekana kupenda baadhi ya vipengele vya Umoja wa Ulaya, wanapinga maamuzi yoyote yanayoonekana kudhoofisha maslahi ya taifa au yenye madhara kwa maisha ya kila siku ya watu wa Ulaya. Kwa mfano, kukiwa na hisia kuwa maamuzi yatakayochukuliwa yatasababisha kupungua kwa ajira kwa raia wa nchi fulani uamuzi huu utapingwa. Matokeo ya utafiti uliofanywa katika nchi za Ulaya unaojulikana kama Eurobarometer Juni mwaka 2005 ulionyesha kwa nini Wafaransa wengi walipiga kura ya "Hapana" kwa katiba ya Ulaya. Baadhi ya sababu zinazotajwa kwa umuhimu wake ni:

1. Katiba ya Ulaya italeta athari katika ajira;
2. Hali ya uchumi ya nchi ni mbaya na kuna ukosefu wa ajira;
3. Katiba ilikuwa ya kiliberali mno;
4. Upinzani kwa serikali na baadhi ya vyama (hasa chama tawala); na
5. Kutokuwa na mipango ya kijamii ya kutosha (Burgio, 2006).

Wasiwasi mwingine ni kuwa ongezeko kubwa la pamoja la wanachama litaleta ugumu katika kuendesha baadhi ya asasi za Umoja wa Ulaya. Tayari sasa hivi, kufuatia ongezeko la tano la wanachama lililohusisha nchi 10, Baraza la Mawaziri la Umoja wa Ulaya limeonya kuwa siku za baadaye halitaruhusu uingizaji wa nchi kwa mafungu bali kila nchi itafanyiwa tathmini inayojitegemea na kuingizwa peke yake. Nchi ambazo zimo kwenye mchakato wa kujiunga na Umoja wa Ulaya na zinakaribia kupata uanachama ni Croatia ambayo inatarajiwa kupatiwa uanachama mwaka 2010, ikifuatiwa na Albania, Bosnia na Hezgovina, Jamhuri ya Macedonia, Montenegro, Serbia na Uturuki. Hapa kinachoongelewa ni kuwa mchakato wenyewe wa kujiunga na Umoja wa Ulaya huchukua muda mrefu na hivyo pengine haitakuwa rahisi tena kwa nchi hizi kuingia katika Jumuiya kwa pamoja. Kama ilivyo utaratibu, itabidi Tume ya Ulaya ifanye tathmini ya maendeleo yanayofikiwa na nchi hizi kuelekea katika viwango vilivyowekwa. Tume ya Ulaya itaandaa ripoti za mara kwa mara na kuziwasilisha kwa Baraza la Ulaya. Baraza la Ulaya litachukua uamuzi kulingana na hali itakavyokuwa kama nchi hizi zipewe uanachama au ziendelee kusubiri mpaka hali ya ndani itakapokuwa imeboreka.

Tunachojifunza kutoka Jumuiya ya Ulaya ni kuwa kwa kiasi kikubwa kila hatua ya mchakato wa kuundwa kwake wananchi walishirikishwa. Njia mbalimbali zilitumika katika kuwashirikisha wananchi kama ilivyokuwa wakati wa kuunda sarafu ya Ulaya (Euro). Kwa baadhi ya nchi kupiga kura ya hapana na kushindwa kujiunga. Hali ilikuwa hivyohivyo wakati wa kukubali Katiba ya Ulaya. Uzuri wake ni kuwa wananchi wanakuwa na umiliki wa Jumuiya kwani vinginevyo ni rahisi jumuiya ikaonekana kuwa ni mali ya viongozi na hivyo kukosa uungwaji mkono wa wananchi. Pakikosekana uungwaji mkono utekelezaji wa mipango ya Jumuiya unakuwa mgumu sana.

Katika manufaa ambayo Umoja wa Ulaya unayapata ni kuimarika kwa sarafu ya Ulaya. Ikiwa na wanachama 12 tu kati ya 27 wanaounda Umoja wa Ulaya, Euro ni moja ya sarafu zenye nguvu kubwa duniani ambayo imekuwa tishio hata kwa dola ya Kimarekani. Inasemekana kuwa hata nchi ambazo hazijajiunga na sarafu hii zinaweza kuvutika na baada ya muda mfupi kujiunga. Pengine funzo kwa nchi za Afrika Mashariki ni kuwa hata katika uamuzi wa kujiunga na sarafu, nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya ziliwashirikisha kikamilifu wananchi wao katika kupitisha uamuzi huo. Uingereza wao wameamua kubaki kwanza nje ya umoja wa sarafu na kuendelea kutumia sarafu yao ya Pauni.

Akichambua faida na hasara za kuwa na sarafu ya pamoja ya Euro Kiflewahid (2004) anazitaja baadhi ya faida kuwa ni:

1. kuondoa uwezekano wa hasara wakati wa kubadilisha pesa;
2. bei kuwa za wazi zaidi;
3. bei kutokubadilikabadilika;
4. kuongezeka kwa biashara;
5. kupungua kwa riba katika mabenki;
6. kutoa ushindani kwa dola kama sarafu ya dunia;
7. misimamo imara katika mazungumzo ya sera za kiuchumi za kimataifa; na
8. sababu za kisiasa (yaani nidhamu katika matumizi ya serikali).

Hasara za kuingia umoja wa sarafu zinatajwa kuwa ni:

1. kupoteza fedha wakati wa kubadilisha, na
2. kupoteza uhuru wa kuamua sera ya fedha.

Funzo kwa nchi za Afrika Mashariki ni kuwa itabidi ziwe na vigezo vinavyoeleweka vya uanachama. Kama nchi haiwezi kufikia vigezo vilivyowekwa, isikubaliwe kujiunga na Umoja. Vigezo kama utawala wa kisheria na wa katiba ni muhimu sana kwa uendelevu wa Jumuiya. Haitawezekana, kwa mfano, kuwa na nchi moja yenye mfumo wa kidemokrasia na nyingine yenye udikteta zikiishi bega kwa bega. Hili halihitaji ufafanuzi mkubwa kwani moja ya sababu ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 ni kuingia kwa udikteta. Vivo hivyo, kwa

sasa itakuwa vigumu kuwa na nchi moja ambayo, mathalani, haitakuwa na kipengele cha ukomo wa vipindi vya urais, wakati katiba za nchi zilizobakia zinatamka wazi kuhusu jambo hilo. Kuingia kwa nchi mpya kutoe fursa ya kuwa na masharti mapya ya kujiunga na Jumuiya. Nchi zinazojiunga pia lazima zipimwe katika vigezo vya uchumi. Ikiwa katika nchi wanachama viwango vyao vya uchumi viko chini sana au ikiwa vina viwango vikubwa vya mfumuko wa bei, zipewe muda wa kuweka sawa mambo na kurekebisha tofauti zilizopo ili kuendana na jumuiya kubwa.

Ongezeko la Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mnamo Julai Mosi 2007, nchi za Burundi na Rwanda zitakuwa wanachama rasmi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo kuongeza wigo wa uanachama kufikia nchi tano. Rwanda ndiyo iliyotangulia kuomba kuwa mwanajumuiya mwaka 1996, ikiwa ni miaka miwili tu tangu nchi hiyo ikumbwe na janga linalosababishwa na binadamu na ambalo limeacha historia mbaya kwenye bara hili. Janga hilo ni mauaji ya kimbari ya 1994.

Burundi nayo ilifikisha maombi ya kuwa mwanachama wa Jumuiya kwa mara ya kwanza mwaka 1998. Kama walivyofanyiwa nchi zinazoomba uanachama kwenye Jumuiya nyingine za kikanda kwingineko, zilipewa masharti ya kuwawezesha kuwa wanachama baada ya nchi anzilishi za Jumuiya kuridhika na dhamira ya uhakika ya serikali za Burundi na Rwanda kujiunga na Jumuiya hiyo. Kwa hiyo nchi hizi zilionyesha kuvutiwa na ajenda ya Jumuiya hata kabla mkataba wa Jumuiya haujaridhiwa na nchi za Kenya, Uganda na Tanzania na kuanza kutumika Januari ya mwaka 2000. Nchi hizi pia zimeingia wakati Jumuiya iko katika harakati za kuimarisha muungano kwa kufikiria kuingia katika shirikisho. Jumuiya imeanzisha taasisi, miradi na mipango mkakati kadhaa, na wakati huohuo ikisimamia zoezi la kukusanya maoni kutoka kwa wakazi wa nchi tatu kuhusu hoja ya kuharakisha shirikisho. Kuingia kwa Burundi na Rwanda kutapelekea mabadiliko mengi ya kiuendeshaji na ya kitaasisi ndani ya Jumuiya. Baadhi ya mabadiliko tutayazungumzia katika sehemu zinazofuata za makala hii pale tutakapokuwa tunajadili changamoto zinazoikabili Jumuiya kwa sasa.

Ni jambo la kufurahisha kuona kuwa Sekretarieti ya Jumuiya imeshaanza

kuzishirikisha nchi za Burundi na Rwanda kwenye shughuli za Jumuiya hata kabla ya kuwa wanachama rasmi kwa minajili ya kurahisisha kipindi cha mpito cha nchi hizo kuelekea kufaidi rasmi haki na wajibu chini ya Mkataba wa Jumuiya. Kwa mfano, hivi karibuni nchi hizo zimeshirikishwa kwenye mikutano ya Jumuiya na kupewa nafasi ya kuwa miongoni mwa ujumbe wa Jumuiya kwenye ziara zilizofanyika Ujerumani, Jumuiya ya Ulaya na India (EAC, 2007). Tayari nchi ya Burundi imepewa kipindi cha mpito cha miaka mitatu (2007-09) kujiandaa kuingia katika ukanda huru wa biashara, na pia kuweka viwango sawa vya ushuru. Mabadiliko ya viwango kwa nchi hiyo yanatarajiwa kuanza Januari 2008.

Jumuiya pia imeanza kutazama upya mkakati wake wa maendeleo (Development Strategy 2006-2010) kwa nia ya kujumuisha maslahi ya wanachama wapya. Hii inamaanisha kutanua miradi kama ya nishati ya umeme, miundombinu kama barabara na reli na miradi mingine ya Jumuiya kwa nchi hizo. Vilevile zoezi la kukusanya maoni ya wakazi wa nchi hizi mbili kuhusu kuharakisha shirikisho itabidi lifanyike siku za usoni. Sambamba na hilo kampeni ya kuitambulisha Jumuiya kwa wadau wa ukanda huu itabidi iwafikie Warundi na Wanyarwanda baada ya nchi zao kujiunga na Jumuiya.

Manufaa ya Ongezeko la Wanachama

Mwaka 2007 utakumbukwa kama ni kipindi ambacho Jumuiya ya Afrika Mashariki ilifanya moja ya maamuzi makubwa katika historia yake kwa kufanya ongezeko la kwanza la wanachama kwa kukaribisha wanachama wapya wawili. Katika sehemu hii tunajaribu kuangalia athari chanya za ongezeko hilo la wanachama. Tunaelewa kuwa Jumuiya inapitia pia kipindi cha ongezeko la majukumu yake. Hivyo basi tutatazama kupanuka kwa wigo wa Jumuiya kiuanachama na kimajukumu kwa pamoja. Ili kurahisisha zoezi hili la uchambuzi tumegawanya manufaa yanayopatikana kwa sasa na yale yanayotarajiwa katika sehemu kuu tatu: kiuchumi, kisiasa, na kijamii.

Kiuchumi, kama ilivyowahi kubainishwa na wachambuzi, watafiti na wasomi mbalimbali wa ukanda huu, mmojawapo akiwa Wangwe (2002:172), nadhari za kiuchumi ndiyo muhimili mkubwa wa ushirikiano wowote wa kikanda. Kushindwa kushughulikia tofauti za kiuchumi na kijamii kama historia inavyoonyesha kumepelekea migogoro iliyosababisha

kuvunjika kwa ushirikiano. Wangwe anatoa mifano ya vita vya wenyewe kwa wenyewe Amerika (1969) na ile kati ya Honduras na El Salvador (1969) kuwa chanzo cha kuvunjika jumuiya katika maeneo hayo. Ni yapi basi manufaa ya kuwa na wanachama watano wa jumuiya?

Kama ilivyogusiwa awali, kuingia kwa Burundi na Rwanda kutaongeza takwimu za kiuchumi kwa Jumuiya kuwa na pato la jumla ya dola bilioni 41 za kimarekani. Pamoja na kwamba sekta ya uzalishaji kwenye nchi hizi bado ni duni, kuunganisha nguvu kiuchumi kutawezesha Jumuiya kuongeza uwezo wake wa kuendesha miradi mikubwa kwa maendeleo ya wanajumuiya. Kuna ukweli usiopingika kwamba miradi mikubwa inayoendelea hivi sasa kama ule wa nishati ya umeme ujulikanao kama East African Power Master Plan na ule wa barabara, yaani East African Road Network Project, inategemea kwa kiwango kikubwa ufadhili wa nje ya Jumuiya. Hata hivyo, kama itakamilika kwa wakati uliopangwa na kwa ufanisi matokeo yake yatakuwa ya moja kwa moja na makubwa. Jumuiya sasa itakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuvutia uwekezaji katika miundombinu inayounganisha nchi-wanachama ambazo kwa bahati nzuri ziko karibu sana kijiografia. Pia nchi wanachama zitafaidika kwa kupunguza gharama zinazoambatana na kuingia mikataba (transactions costs). Jambo la kusisitiza hapa ni kwamba faida ya kuunganisha nguvu na kuanzisha miradi itaonekana zaidi kama miradi hiyo itachochea ukuaji uchumi wa nchi husika kutokana na upatikanaji ajira na kuboreka kwa hali za wakazi wa Jumuiya kwa ujumla.

Ili kutekeleza baadhi ya malengo ya ushirikiano wa kikanda, Jumuiya imeainisha maeneo kadhaa yenye manufaa kwa wanajumuiya wote ili yasimamiwe kwa pamoja na kwa ukaribu zaidi. Eneo mojawapo ni Ziwa Victoria na eneo linalolizunguka ambalo linachukua kilomita za mraba 193,000 katika nchi za Kenya, Tanzania na Uganda na sehemu za Burundi na Rwanda. Eneo hili ambalo pia hujulikana kama Lake Victoria Basin linakaliwa na asilimia 40 ya watu wa ukanda huu na pia linachangia asilimia 50 ya pato kwa watu wake (Nyanjom, 2005). Bonde hili ambalo ndilo chanzo cha mto Nile lina fursa nyingi za uwekezaji kwa sekta za uvuvi, utalii, usafiri na uchukuzi, maji na nishati, kilimo, biashara na viwanda. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika hivi karibuni, kisiwa cha Ukerewe pekee kina vivutio vya kitalii zaidi ya 500 ikiwemo moja ya mandhari bora kabisa

duniani ya mithali ya kutua kwa jua (Daily News, Desemba 2, 2006). Kwa kutambua umuhimu wa bonde hili nchi wanachama walipitisha Hati inayohusu maendeleo endelevu ya eneo hilo mnamo Novemba 30, 1999. Kuingia kwa Burundi na Rwanda kunaongeza umuhimu wa Hati hiyo. Ikumbukwe kwamba nchi zinazounda Jumuiya pia ni wanachama wa ushirikiano chini ya chombo kiitwacho Nile Basin Initiative (NBI) chenye wanachama kumi. Hii itawapa nafasi wanajumuiya kuwa na sauti moja kwenye chombo hiki.

Kibiashara, nchi wanachama wapya zinatarajia kunufaika na kuunganishwa na miundombinu ya nchi za Jumuiya na hivyo kupunguza gharama za uchukuzi (IMF, 2007). Kuingia kwa Burundi na Rwanda kutarasimisha biashara miongoni mwa nchi hizo na nchi tatu waanzilishi wa Jumuiya ambayo imekuwa ikiendelea hata wakati nchi hizo zilipokuwa katika kipindi kigumu kisiasa.

Katika nyanja za kisiasa yapo manufaa kadhaa yanayotarajiwa. Tangu mwaka 2005 Jumuiya ilishaanza kuzungumzia uwezekano wa kushirikiana katika ngazi ya kidiplomasia il nchi wanachama wa Jumuiya wawe na msimamo mmoja kwenye mikutano na hafla za kimataifa. Linginc lililoanza kuwekewa mkakati ni kushauriana kabla ya kusimamisha wagombea wa nyadhifa katika mashirika ya kimataifa ili kuepusha ushindani baina yao kwa nafasi zilizotengwa kikanda au za kisiasa. Vilevile imeshazungumzwa haja ya kushirikiana kutoa huduma za kibalozi miongoni mwa wanachama. Ikiwa haya yatafanyika kama nia ya wafanya maamuzi ilivyo, basi wanajumuiya wataongeza mshikamano wa kisiasa. Ushirikiano huu utaimarika zaidi baada ya kutengenezwa sera ya mambo ya nje na usalama. Hivi sasa kuna makubaliano kuhusu sera ya nje ambayo bado hayajapandishwa hadhi ya kuwa hati. Ipo pia kamati inayohusika na sekta hii ambayo inaripoti kwa Mkutano wa Mawaziri wanaoshughulika na Jumuiya.

Mchakato wa kutengeneza kanuni za Jumuiya zitakazotoa mwongozo kwa uendeshaji wa chaguzi za kidemokrasia na kuunda kamati ya utawala bora umesitishwa baada ya Kenya na Uganda kupendekeza kwamba bado ni mapema na kuwa suala hilo lianze kufikiriwa baada ya kukamilika kwa sera ya pamoja ya mambo ya nje. Hili ni eneo lingine muhimu sana hasa Jumuiya inapoelekea kwenye hatua za juu za ushirikiano. Mkutano wa

Wakuu wa Nchi umesharidhia hatua ya kufungua ofisi ya Jumuiya katika makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU) itakayoratibu masuala ya amani na usalama. Masuala ya amani na usalama yanajadiliwa kwa kina katika mfululizo wa makala nyingine.

Inatarajiwa pia kuwa kuingizwa kwa Rwanda na Burundi kwenye Jumuiya kutasaidia katika kuimarisha mahusiano ya Jumuiya na nchi zinazozungumza Kifaransa ikiwamo Ufaransa yenyewe. Nchi nyingi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikuwa na uhusiano mzuri na Uingereza pamoja na Jumuiya ya Madola kuliko nchi za Kifaransa. Pengine hii itatoa fursa nzuri zaidi za kuongezeka kwa mwingiliano na nchi zinazoongea Kifaransa. Kwa upande wa Kenya, Uganda na Tanzania itabidi zitilie mkazo mipango yake ya kufundisha Kifaransa mashuleni ili kurahisisha mawasiliano.

Kwa kiasi kikubwa inatarajiwa kuwa kujiunga kwa Rwanda na Burundi katika Jumuiya kutasaidia sana kubadili hali katika nchi hizi. Itakumbukwa tu kuwa Rwanda na Burundi ni nchi ambazo zimeendelea kukumbwa na migogoro ya kikabila ya muda mrefu. Hata wakati fulani Rais mstaafu wa Kenya Daniel Arap Moi alinukuliwa akisema dawa ya kudumu ya mgogoro wa Burundi na Rwanda ingekuwa kuzifanya nchi hizo sehemu ya Tanzania au Kenya. Hata kama matamshi haya yalichukuliwa kuwa yalikaribia kudhalilisha utaifa wa nchi hizi mbili, yanayojiri hivi sasa ni kielelezo kuwa umuhimu wa nchi kuungana bado upo palepale. Kwamba angalau kuna ukweli kwa alichokisema Moi hasa upande wa usuluhishi wa mgogoro. Burundi na Rwanda zina makabila makubwa mawili ambayo yamekuwa yakipigania madaraka ya dola kwa maslahi finyu ya kikabila. Jumuiya ya Afrika Mashariki itasaidia kuwa 'nguvu ya tatu' na hivyo kupunguza siasa za ukabila katika nchi hizi.

Manufaa ya ongezeko la wanachama kijamii yana uhusiano wa karibu na yale ya kiuchumi na kisiasa. Hapa tunaongeza mambo makubwa mawili: moja, ni mwingiliano mkubwa zaidi wa kiutamaduni na ubadilishanaji wa stadi za maisha ya wakazi wa Jumuiya. Hofu iliyoanza kujengeka hasa wakati huu wa kukusanya maoni kuhusu kuharakisha shirikisho kuwa tamaduni za nchi jirani zitavuruga za kwetu pengine zimeangalia zaidi upande mmoja. Kwa hali ya kawaida hakuna utamaduni ambao unaweza kujisifu kuwa una mambo mazuri tu na hivyo hauwezi kujifunza kutoka nje. Vivo

hivyo, tamaduni mbalimbali zikija pamoja hutegemewa kuwa yale mazuri kutoka pande zote yatachukuliwa na kuendelezwa na yale mabaya yataachwa. Hatimaye, utakuja kujengeka utamaduni wa Jumuiya.

Nchi za Burundi na Rwanda zimekubali kujiunga na Jumuiya inayotumia lugha za Kiingereza na Kiswahili katika shughuli zake. Tayari mpaka sasa nchi waanzilishi wa Jumuiya wamefikia hatua ya kukubaliana juu ya Hati ya Baraza la Kiswahili la Jumuiya. Lugha ni kiunganishi muhimu sana kwenye ushirikiano wa aina yoyote, hususan kwa wadau wa Jumuiya ambao ni wakazi wa ukanda huu. Cha kutia moyo ni kuwa Kiswahili kinazungumzwa katika nchi hizi zote ingawa kwa viwango tofauti. Faida nyingine inaweza kuwa lugha ya Kifaransa itapata msukumo mkubwa zaidi katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania ambazo ziliweka mkazo kwenye Kiingereza.

Kwa muda mrefu sasa nchi hizi zimekuwa zikiandaa mashindano ya michezo mbalimbali. Mashindano yenye msisimko mkubwa zaidi ni yale ya mpira wa miguu yanayojulikana kama Kombe la CECAFA au Kagame Cup ambayo yamekuwa yakifadhiliwa na Rais Paul Kagame wa Rwanda kwa miaka kadhaa sasa. Mashindano haya yamejumuisha nchi zote tano zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa. Hivyo, tunaweza kusema ushirikiano wa kijamii katika ukanda huu ulianza mapema zaidi.

Changamoto Zinazotokana na Kuongezeka Wanachama

Changamoto kwa Jumuiya

Pamoja na nia nzuri za kuunganisha nguvu kwa lengo la kujenga Jumuiya endelevu yenye kuleta manufaa kwa nchi wanachama bado kuna changamoto kubwa zinazokabili Jumuiya hivi sasa na nyingine zinatarajiwa kujitokeza siku za usoni. Kwa mujibu wa ibara ya 5 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, "malengo ya kuunda Jumuiya ni kuweka sera na mipango yenye nia ya kupanua na kuimarisha ushirikiano wa nchi wanachama katika nyanja za siasa, uchumi, jamii na utamaduni, utafiti na teknolojia, ulinzi, usalama na masuala ya sheria, kwa manufaa ya kitaasisi." (tafsiri yetu). Kama inavyoonekana malengo haya yametanda kwenye eneo kubwa la ushirikiano. Jinsi wigo wa ushirikiano unavyokuwa mkubwa

ndivyo changamoto zinavyoongezeka. Suala si kwa nchi wanachama ama kuziogopa, kujisahaulisha, au kuzikimbia changamoto bali ni kuwa tayari kuzikabili kwa umakini mkubwa, na kwa kushughulikia viini vyake, kwa wakati muafaka. Katibu Mkuu wa kwanza wa Jumuiya ya Afrika, Balozi Francis Muthaura, aliwahi kubainisha changamoto zifuatazo zinazoikabili Jumuiya:

Utashi wa Kisiasa na Uungwaji Mkono na Wanachama

Utashi wa kisiasa ni muhimu sana kwa Jumuiya kuendelea kuwepo. Kuna wakati ambapo viongozi wa nchi hukimbilia katika kuunda miungano ya kikanda kama tu "danganya toto" ili kutimiza malengo yao finyu ya kisiasa. Hutokea kuwa baada ya kukamilisha malengo yao viongozi wa namna hii huitelekeza hoja ya kuungana. Hili limewahi kutokea mara kadhaa na hata wasomi wengine wanadhani sababu kubwa ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 ilikuwa ni kukosekana kwa utashi wa kisiasa. Lakini, vilevile, kwa kuwa hizi ni nyakati za demokrasia ya ushirikishaji, ni muhimu kwa Jumuiya kupata uungwaji mkono wa wananchi wa nchi hizi kwa ujumla. Tumeshuhudia Jumuiya nyingine za kikanda zikipoteza wanachama baada ya nchi kuona kuwa hazipati maslahi yoyote kwa kuwa kwao ndani ya Jumuiya husika. Kwa Jumuiya kama ya Afrika Mashariki yenye wanachama wachache, changamoto kubwa ni kuvutia wanachama wengi zaidi na sio kuwapoteza waliopo. COMESA na ECOWAS, mathalani, zina wanachama zaidi ya 20 kila moja. Tusije tukafikia mahali tunafunga 'harusi kubwa' ya ushirikiano kwa mbwembwe nyingi na vifijo wakati baadaye 'tunatalikiana' kimyakimya au kwa kunyosheana vidole.

Kuoanisha Ushuru wa Forodha

Changamoto hii inawezekana imejitokeza mapema zaidi ya nyingine zilizotajwa kwenye makala hii. Ushuru wa forodha una athari kwenye mapato ya nchi husika na ndio maana umekuwa moja ya masuala tete kwenye mazungumzo ya wanachama watatu wanzilishi wa Jumuiya.

Itakumbukwa kuwa suala hili lilipelekea utiaji saini Hati ya Umoja wa Forodha kuahirishwa mara tatu. Na ilipofika Septemba 15, 2005 Baraza la Mawaziri wa Jumuiya wakachapisha Notisi (Legal Notice No. 1) ambayo ilikuwa imefanya marekebisho kadhaa na kutoa ufafanuzi wa viwango vya ushuru chini ya utaratibu uitwao Harmonised Community Desciption and Coding System. Katika mwaka wa kwanza tangu kuanza kutumika umoja wa ushuru wa forodha, kumekuwepo na baadhi ya vigingi. Iliripotiwa siku za hivi karibuni kuwa sukari ya Uganda ilizua kasheshe Kenya, na kwamba "kuna wakati maziwa kutoka Uganda yalizuiliwa kuingia Rwanda" (Kasaija, 2004:31).

Suala la ushuru wa forodha linaumiza vichwa zaidi kwa kuwa sheria inayoisimamia, yaani the East African Customs Management Act (2004) inaeleza kuwa nchi moja isiwe mshiriki wa zaidi ya umoja wa ushuru wa forodha mmoja. Kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.3 nchi tano zinazounda Jumuiya zinashiriki kwenye Jumuiya nyingine za kikanda zilizo kwenye mipango tofauti ya umoja wa forodha. Suala lingine linaloongeza chachu ya changamoto hii ni ushiriki wa nchi wanachama kwenye meza ya mazungumzo na Umoja wa Ulaya kwa kupitia migongo tofauti ya Jumuiya zao za kikanda. Hili tumelizungumzia japo kwa ufupi kwenye orodha ya pili ya changamoto, iliyoko sehemu hii.

Ugharamiaji wa Pamoja wa Taasisi, Mipango na Miradi ya Jumuiya

Pengine hii ndiyo changamoto inayoweza kufifisha jitihada za Sekretarieti ya Jumuiya kuleta mabadiliko yanayokusudiwa kama itashughulikiwa kijuujuu. Kadri Jumuiya inavyopanuka inalazimu kufanya mabadiliko katika muundo wa Jumuiya yenyewe. Mabadiliko ya muundo hasa yanayohusisha kuongeza wigo yanagusa pia vyombo vya maamuzi na taasisi zake. Na kwa kuwa taasisi huendeshwa na watu suala la ajira mpya ni kitu cha kawaida. Mambo haya yote yanagusa suala la bajeti ya Jumuiya ambayo kwa sasa inategemea sana michango ya sawa kutoka kwa nchi wanachama. Nchi wanachama zimekuwa zikitoa michango yao kwa awamu badala ya mkupuo mmoja na mara kadhaa wamechelewa kulipa karisaji zao (EAC, 2004: 66). Zinapochelewa kuchangia kasma ya Jumuiya ndivyo

zinavyokwamisha kazi za Sekretarieti na hatimaye Jumuiya. Kwa sasa mapendekezo ya njia nyingine za kuchangia bajeti ya Jumuiya yamewekwa kapuni mpaka 2010 ikionekana ni "mapema mno" kujaribu utaratibu mbadala.[1]

Hata hivyo, shughuli za Jumuiya zinaendeshwa kwa programu yenye kalenda. Hivi karibuni Sekretarieti ilikamilisha mchakato wa kuajiri wafanyakazi wapya 22 kwenye nafasi mbalimbali kutokana na dharura ya uwazi wa nafasi na kuongezeka kwa shughuli za Jumuiya. Ikitumika kanuni ya urari wa michango kutoka nchi wanachama katika nafasi 12 kati ya hizo iliamuliwa wapewe kipaumbele waombaji toka Burundi na Rwanda. Ujio wa Burundi na Rwanda ulipodhihirika zilijitokeza hoja ndani ya Jumuiya kubadilisha muundo wa Sekretarieti ili uongozi wake uwe na uwakilishi wa wanachama zaidi ya ilivyo sasa. Baada ya kushindwa kukubaliana, wanachama wameamua kuajiri mtaalam wa kutazama na hatimaye kupendekeza muundo mpya. Vyovyote wanachama watakavyokubaliana baada ya kupokea mapendekezo ya mtaalam huyo suala la gharama halikwepeki. Hata kuajiri mtaalam wa kuishauri Jumuiya, pamoja na nia njema ya kuondoa mkwamo wa kufikia maamuzi, ni moja ya namna ya kuongeza gharama za uendeshaji.

Kadri Jumuiya inavyopanuka, taasisi za uendeshaji nazo pia zinaongezeka. Siku zijazo itabidi chombo muhimu kama Bunge la Jumuiya kuongeza wajumbe, na hilo litagusa posho na marupurupu. Gharama ya demokrasia kupitia chombo hiki itakwenda juu pale Jumuiya itakapoamua wabunge wa Bunge la Jumuiya wachaguliwe na wakazi wa Afrika Mashariki badala ya utaratibu wa sasa kama ilivyobainishwa kwenye mkakati wa tatu wa maendeleo wa Jumuiya (2006-2010). Labda mzigo wa gharama ya kuwapata wabunge urudishwe kwa Tume za uchaguzi za nchi husika lakini bado mzigo unabaki kwa nchi wanachama. Mkutano wa 13 wa Mawaziri wanaoshughulika na masuala ya Jumuiya uliofanyika Novemba 2006 uliamua kuwapa majaji wastaafu wa EACJ, Jaji Warioba na Jaji Bossa, honoraria ya kiasi cha dola za kimarekani 15,000 kila mmoja na kupendekeza utaratibu huo urasimishwe. Mkutano huo pia uliiagiza Sekretarieti kutumia kiasi cha dola za kimarekani 161,000 kwa kutafuta

wimbo wa Jumuiya. Mazoezi haya ni gharama ambazo nchi wanachama lazima wakubali kuzibeba bila kusita.

Ukuaji Endelevu wa Uchumi katika Nchi Wanachama

Si jambo la kuficha kuwa Jumuiya za kikanda za zama hizi zinategemea mhimili wa kiuchumi. Kama uchumi wa nchi wanachama ni duni, au haitabiriki kwa maana ya kuelekea kupata ahueni leo na mwaka ujao kuwa hoi, hali ya kifedha ya Jumuiya itakuwa taabani na hatimaye kupelekea kushindwa kuhudumia miradi yake lukuki. Mwishowe ujasiri wa wanachama katika kuchangia zaidi ya nusu ya bajeti utayeyuka mpaka kiasi cha kuhamishia utegemezi wa wahisani kwenye ngazi ya Jumuiya ya kikanda. Tunaomba hilo lisitokee Kwani itakuwa ni fedheha ya kimataifa.

Kupoteza Mamlaka ya Dola

Kama tulivyokwishaona huko nyuma kwa kuangalia mfano wa Umoja wa Ulaya, nchi zinapokubali kuungana hazina budi kukubali kuachia baadhi ya mamlaka ya dola na kuyahamishia katika jumuiya itakayoundwa. Lakini mara nyingi utekelezaji wa suala hili huwa mzito kwa sababu aghalabu nchi hazipendi kupoteza mamlaka yake. Tumeona, kwa mfano, Waingereza bado wanajivuta kuingia katika Umoja wa Sarafu ingawa ni dhahiri kuwa huko mbele watalazimika kuingia. Kwa hapa kwetu hali hii imeshaanza kujitokeza na kuonekana inatoa changamoto kwa Jumuiya. Ugumu unaweza kujitokeza pale ambapo maslahi ya makundi mbalimbali ya wadau wa nchi husika kama vile wafanyabiashara, wakulima, wawindaji, wavuvi, wafugaji, wafanyakazi, wataalam, na kadhalika, yatakapoathirika kwa watawala kurekebisha sera au kuridhia mikataba itakayohatarisha au kupunguza maslahi yao. Watawala kwa upande wao hawatakuwa tayari kunyimwa fursa ya kuyatumikia makundi yote ya wadau na jamii nzima kwa kupewa adhabu kwenye sanduku la kura. Mathalani, hapa Tanzania tumeona wadau wa sekta ya mahoteli ya kitalii walivyopinga mwanzoni namna utaratibu wa kuweka alama za ubora kwa vitega uchumi vyao wakisukumwa na haja ya kulinda maslahi yao.

Kinadharia, ni vigumu kwa nchi wanachama wa ushirikiano wa namna yoyote kuwa na mtazamo mmoja dhidi ya masuala mbalimbali na hasa yale yanayogusa maslahi yao. Changamoto ni kuweka utaratibu na mikakati ya kupunguza tofauti za kisera, ili kuepusha mpasuko na migogoro ndani ya Jumuiya. Awali, nchi wanachama zimewahi kuchukua maamuzi yaliyoonekana kupingana. Ripoti ya Kamati ya Wako imetoa mifano michache ya siku za hivi karibuni pale ambapo Kenya ilipoweka Simba kwenye orodha ya wanyama walio hatarini kutoweka wakati Tanzania inahamasisha uwindaji wa Simba. Suala lingine ni matumizi ya maji ya mto Nile na utunzaji wa Ziwa Victoria.

Kuna suala nyeti la mazungumzo yanayoendelea baina ya Umoja wa Ulaya (EU) na Jumuiya kadhaa za kikanda barani Afrika yakijulikana kama Economic Partnership Agreements (EPAs). Baadhi ya nchi tayari zimekwishajikuta njia panda. Mathalani, Tanzania kwa zaidi ya miezi 13 imeshindwa kufikia hatua nzuri ya mazungumzo baina yake na EU kuhusu EPA. Hii ni kwa sababu Tanzania pia ni mwanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo pia iko katika mazungumzo na EU kuhusu EPA. Je ijitoe SADC ili ifanye makubaliano kupitia Ushuru wa forodha wa Afrika Mashariki, au kupitia kundi la East and Southern Afrika? Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko wa Tanzania, Basil Mramba, aliwahi kunukuliwa akisema kuwa kitendawili kikubwa kinachoikabili Tanzania na nchi kama Angola na Msumbiji kimekuwa si kufanya makubaliano ya EPA, bali ni kutatua suala la uanachama kwenye mashirikiano ya kikanda[2] (The East African, Aprili 3, 2007). Inasemekana kuwa Kenya na Uganda zinasita kuijadili EPA kupitia EACU, na hivyo kuiacha Tanzania njia panda. Mwaka 2003 SADC ilipendekeza Tanzania iendelee kujadili EPAs kupitia SADC.

---

[1] Sura ya 28, kifungu cha 132(4) cha Mkataba wa Jumuiya kinaeleza kuwa fomyula ya kulipia bajeti ni michango sawa toka kwa nchi wanachama ingawa inatoa nafasi pia kwa michango ya wafadhili na wahisani wengine.

Utekelezaji wa maamuzi ya Jumuiya

Ili Jumuiya ifanye kazi zake vizuri na hatimaye ipate uungwaji mkono na wanachama, itakuwa muhimu kwa maamuzi nyeti kutekelezwa kwa muda uliopangwa. Mara nyingi vyombo mbalimbali vya Jumuiya vinaweza kutoa maamuzi kuhusu mambo kadhaa lakini kinacholeta tofauti ni utekelezaji wake. Kwa kuwa maamuzi haya hugusa eneo kubwa zaidi katika nchi tofauti pengine hutokea Sekretariati ikacheleweshe utekelezaji wa maamuzi. Moja ya malalamiko ndani ya Umoja wa Ulaya ni kuwepo urasimu katika Tume ya Ulaya. Kuna haja ya kuhakikisha kuwa hili halitokei kwa Jumuiya yetu hasa kipindi hiki ambapo taasisi zake zinaongezeka kwa idadi na majukumu. Hili tunalowakilisha hapa lisichanganywe na gharama (za muda na fedha) za kutumia haki ya kidemokrasia ya kulalamika, au kutafuta haki pale mambo yanapofanywa kinyume na mkataba wa Jumuiya. Pale baadhi ya wakazi wa Jumuiya hii walipoona kuna 'faulo' imechezwa katika kupata wawakilishi wao, wafanya maamuzi hawakusubiri sana kupendekeza marekebisho ya 'chapuchapu' kwenye sheria inayoendesha mahakama ya Jumuiya.

Kulinda Amani na Usalama

Mkataba wa Jumuiya unatambua umuhimu wa amani na usalama kwa maendeleo ya Jumuiya yenyewe na wanachama wake. Ramani ya Jumuiya imepanuka wakati hali bado haijawa shwari kwa wanachama wote. Vitendo vyovyote vya uvunjaji amani na usalama wa eneo lolote ndani ya Jumuiya ni saratani kwa uhai na maendelec ya Jumuiya. Kuibiana ng'ombe, kuchomeana nyumba, kuuana na kadhalika visingoje kalenda bali vinatakiwa kudhibitiwa mara moja kwa pamoja. Ukanda huu nao unatakiwa useme basi kwa zoezi la kudhalilisha, la kuzalisha wakimbizi. Kama juhudi za siku zijazo za kuwa na mwenendo unaofaa wa utawala wa kisheria ndani ya wanachama zitakwama, basi tusije kushangaa serikali husika zikiongeza bajeti ya kununua silaha huku zikichechemea kuchangia bajeti ya Jumuiya.

Uwezo wa Kubeba Majukumu

Kuna hatari ya Jumuiya kujibebesha mzigo mkubwa ambao unaweza kuja kuishinda huko baadaye. Tunavyoona kwa sasa Jumuiya imejiwekea muda mchache sana katika kutekeleza maamuzi muhimu ya mustakabali wa nchi wanachama. Wakati bado utekelezaji wa Umoja wa Forodha haujashika

kasi ya kutosha, tayari Jumuiya inafikiria kuanzisha shirikisho. Wakati huohuo kuna uamuzi wa kuingiza wanachama wapya. Inasemekana kuwa kinachoisibu Jumuiya ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) leo hii ni 'kutekwa' na operesheni za kijeshi na 'kulewa' sifa za kazi nzuri iliyofanya kule Liberia na Sierra Leone, na hatimaye kuzorota kwa shughuli za kiuchumi kulingana na malengo yaliyo ndani ya mkataba wa Jumuiya hiyo.

Kuondoa hali ya wasiwasi na woga kuhusiana na mambo mbalimbali miongoni mwa wakazi na wadau wa Jumuiya

Mbali ya kutoielewa Jumuiya na shughuli zake vizuri wakazi wengi (haswa kutoka Tanzania) wa ushirikiano huu wa kikanda wameonyesha wasiwasi wa kupoteza ajira, soko na ardhi kutoka kwa wakazi wa nchi wanachama wengine. Pia umejitokeza wasiwasi wa kukinzana kwa stadi za maisha na tamaduni. Wasiwasi huu wa wakazi, ama uwe wa kweli au wakiutambuzi ni changamoto kubwa kwa Jumuiya na wanachama wake. Imezungumzwa na Wakuu wa Nchi wanachama mara kadhaa kuwa wakazi wa Jumuiya ndiyo nguzo ya ushirikiano wa kizazi hiki cha Jumuiya za kikanda, hivyo basi bila kuweka juu imani ya wakazi kuhusu Jumuiya, hakutakuwa na nguzo ya ushirikiano kwa uhalisia wake.

Kukabiliana na changamoto zinazotokana na kuwa na Jumuiya kubwa yenye sauti kisiasa na nguvu ya kiuchumi

Tukiangalia upande mwingine wa shilingi Jumuiya hii inayojengwa ukanda huu yaweza kuibuka kuwa mhimili muhimu wa kiuchumi na chombo adhimu katika siasa za kimataifa kama mambo yote yatakuwa sawia. Hii itamaanisha kupungua kwa uwezo wa mataifa makubwa na mashirika ya kimataifa kuyumbisha nchi za ukanda huu kwa maslahi yao. Changamoto inayotokana na hali hiyo ni kukabiliana na upinzani dhidi ya 'jumuiya imara' iliyoasisiwa na kulelewa vilivyo na ushirikiano wa nchi zinazoendelea. Upinzani huo utakaopata msukumo nje ya jumuiya utafanya kazi moja kuu: kugeuza masahibu wa ushirikiano wa kikanda kuwa maharamia wa ushirikiano wa kikanda. Kama ilivyodokezwa kwenye ripoti ya Kamati ya

Wako, upinzani unaweza kuchochewa kwa njia kadhaa ikiwemo 'kufadhili' kampeni dhidi ya Jumuiya na kukebehi hatua zozote za ushirikiano zionekane kama 'ndoto za alinacha'!

Changamoto kwa Wanachama Wapya

Kufuatia uamuzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Novemba 30, 2006 mjini Arusha, nchi za Burundi na Rwanda zilikubaliwa kuwa wanachama wa Jumuiya. Uanachama wao ulianza rasmi Julai Mosi 2007 mara baada ya kutimiza masharti yaliyopo kwenye mkataba wa kuingia uanachama ujulikanao kama Accession Treaty. Kuingia kwa nchi hizi kutapelekea marekebisho katika Mkataba wa Jumuiya. Hata hivyo, kama ilivyo kwenye Jumuiya ya Ulaya, wanachama hawa wapya itabidi wakubaliane na yale yote yaliyokwisha kukubaliwa na Jumuiya mpaka siku wanapoingia rasmi, ama kwa lugha ya kitaalamu ijulikanayo kama the acquis communautaire. Hii inamaanisha pia kuwa nchi hizo zinakuwa na haki na wajibu kama wanachama wengine ndani ya mkataba wa Jumuiya. Vilevile zinabidi ziheshimu sheria zaidi ya 13 zilizopitishwa na Bunge la Afrika Mashariki tangu 2002; hati na mikataba takriban 15 iliyofikiwa mpaka hivi sasa. Hati na mikataba hiyo inagusa maeneo yafuatayo:

- Kuzuia ulipaji kodi mara mbili na ukwepaji wa kodi;
- Utoaji maamuzi wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya;
- Kupambana na usafirishaji madawa ya kulevya katika ukanda huu;
- Masuala ya viwango na ubora wa bidhaa;
- Usafiri wa barabara;
- Usafiri wa ndani wa majini;
- Kuanzisha Baraza la Vyuo Vikuu la Afrika Mashariki (Inter University Council for East Africa);
- Masuala ya upekuzi na uokoaji;
- Mazingira na maliasili;
- Uanzishaji wa Tume ya Sayansi na Teknolojia;
- Uanzishaji wa Taasisi ya Usalama wa Anga;
- Uanzishaji wa Kamisheni ya Kiswahili; na
- Uanzishaji wa kamisheni ya Utafiti wa Afya.

Changamoto ya kuongezeka kwa wigo wa uanachama pengine ilionekana vizuri zaidi katika Umoja wa Ulaya tangu ikiwa na wanachama ilipofanya ongezeko la kwanza. Tofauti za kiuchumi za wanachama wapya zilipelekea Umoja huo kuweka vigezo tofauti vya kujiunga na Umoja (Harrop, 2000 kama alivyonukuliwa kutoka Shams, 2002:87). Ongezeko la wanachama wa EU pia limeongeza ugumu wa taratibu za kufikia maamuzi na hivyo Umoja huo ukatanua utaratibu wa kupiga kura kwa masuala mengi zaidi na kufanya mabadiliko katika utaratibu wa "kura ya uzito" ili kuepusha kushindwa kufikia maamuzi (Shams, 2002). Tofauti za hali za wanachama wapya ilipelekea kuamuliwa kuanzisha mfuko uitwao Cohesion Fund kwenye mkataba wa Maasticht wa Februari 1992. Mfuko huu ulilenga kuzisaidia nchi za Hispania, Ureno, Ugiriki na Ireland kuanzisha miradi inayohusiana na miundo ya usafiri na mazingira (Holthus, 2002: 97).

Ingawa nchi za Afrika Mashariki nazo zimeamua kuanzisha mfuko uitwao EAC Partnership Fund, mfuko huu haukusudii kwa kusaidia wanachama wapya pekee kama ulivyo ule wa EU bali ni kusaidia kugharamia miradi ya Jumuiya. Mfuko huu kama jina lake lilivyo unategemea zaidi ufadhili wa nje. Kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 "Washirika wa Maendeleo" walitoa dola za kimarekani milioni 2 na kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 wameshatoa kiasi cha dola za kimarekani milioni 4 kusaidia miradi na mipango ya Jumuiya. Hivyo nchi za Burundi na Rwanda zisitarajie upendeleo wa makusudi kama ule uliofanywa na EU kwa wanachama wake wapya. Wanachama hawa wapya wana changamoto kubwa, kwanza ya kwenda na kasi ya utekelezaji wa maamuzi na mikataba iliyofikiwa na wanachama waanzilishi. Pili, wana kazi nzito ya kuweka mwenendo wa uchumi wa mataifa yao katika mazingira mazuri ya kuweza kushindana na wanachama wengine. Ikumbukwe kuwa nchi hizi zitatoa ada ya uanachama kama nchi nyingine za Jumuiya. Watawala wa nchi za Burundi na Rwanda wakijua hilo wajiandae vyema kuingia rasmi kwenye ushirikiano lakini wenye "kinyang'anyiro" cha uchumi huria ambapo sasa ile hofu ya kumezwa kiuchumi ni dhahiri zaidi kwao kuliko nchi kama Tanzania na Uganda.

Changamoto kwa Wanachama Waanzilishi

Mbali ya changamoto kadhaa tulizozitaja hapo juu tunadhani zipo zile zinazozihusu pekee wanachama wanzilishi wa Jumuiya. Kuna haja kwa

nchi hizi tatu (Kenya, Tanzania na Uganda) kuzikaribisha kwa mikono miwili nchi za Burundi na Rwanda. Kwa kusema hivi tunamaanisha nini? Mikutano imefanyika, maamuzi yametiwa saini, na mvinyo wa kupongezana umenywewa, sasa ni muda wa kudhihirisha kimatendo usamaria wetu kwa nchi hizi mbili. Kwa maoni yetu tutakuwa tunakanganya mambo ikiwa vitendo na kauli za ama viongozi, wanasiasa au watendaji wetu kwenye Serikali na ndani ya Jumuiya vinaendana kinyume na 'mkono wa karibu' tuliowanyooshea wenzetu. Tunafikiri juhudi zifanywe kuweka hali ya mshikamano ili kutufanya tusahau mapema sana misamiati ya "Wanachama Wapya" na "Wanachama Waanzilishi" badala yake tuseme Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwani uanachama kwenye jumuiya za kimataifa si kama uraia wa kuandikisha/kuomba.

Hitimisho

Katika makala hii tumeangalia manufaa na changamoto za kuongezeka kwa wanachama wapya wa Jumuiya. Tumetumia mifano mingi kutoka Umoja wa Ulaya kwa sababu tunadhani Umoja wa Ulaya ni moja ya Jumuiya iliyojengeka hatua kwa hatua na imeendelea kupokea wanachama wapya tokea kuanzishwa kwake. Manufaa ya kuongezeka kwa wanachama yameangaliwa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kisiasa tumeona kuwa ongezeko la wanachama litamaanisha kuasisiwa kwa umoja mkubwa zaidi wenye watu wengi. Maana yake ni kuwa katika siasa za kimataifa kwa pamoja nchi hizi zitakuwa na sauti kubwa zaidi. Pengine zitakuwa ni mifano ya nchi chache za Kiafrika zilizoungana. Pili, inategemewa kuwa kuongezeka kwa Rwanda na Burundi kutaiweka Jumuiya karibu zaidi na nchi zinazoongea Kifaransa na hivyo kunufaika na upande huo. Tunaona kuwa kabla ya hapo nchi hizi zilikuwa na ukaribu na Uingereza na nchi za Jumuiya ya Madola kuliko ilivyokuwa kwa nchi za Kifaransa. Kiuchumi inategemewa kuwa kupanuka kwa Jumuiya kutamaanisha soko kubwa zaidi. Wawekezaji hushawishika kuwekeza mitaji yao wakiridhika kuwa kutakuwa na soko la uhakika la bidhaa na huduma zao. Hivyo Jumuiya itawezesha uwekezaji mkubwa zaidi wa mitaji na hivyo kuimarisha sekta nyingine za uchumi. Kijamii kuingia kwa Rwanda na Burundi

kutaimarisha mahusiano ambayo yamekuwepo baina ya nchi hizi. Tumeona kuwa hata kabla ya kujiunga na Jumuiya, nchi za Rwanda na Burundi zilitegemea Bandari ya Dar es Salaam na Mombasa kupitisha bidhaa zao. Nchi za Afrika Mashariki pia zimekuwa kimbilio kwa wakimbizi wa Rwanda na Burundi na hivyo kuzifanya kuhusiana kijamii. Tanzania, mathalani, imekwishatoa uraia kwa wakimbizi wa Rwanda na Burundi siku zilizopita na vivyo hivyo kwa Uganda.

Changamoto za kuongezeka wanachama zipo nyingi. Kati ya tulizozichambua ni pamoja na changamoto za kurekebisha uchumi na kuoanisha sera za nchi hizi. Tumeona kuwa kwa kuja pamoja nchi hutakiwa kuwa na mwelekeo unaofanana sio tu wa kiuchumi bali pia wa kisiasa na kijamii. Kwa hivyo changamoto kubwa ni kuhakikisha kuwa uchumi wa Rwanda na Burundi unakuwa katika kasi ya kuridhisha kufikia viwango vya nchi wanachama wa Jumuiya. Pamoja na kuwa nchi hizi hazina uchumi mkubwa wa kujivunia, lakini hali ni nafuu kidogo ukilinganisha na Rwanda na Burundi. Tofauti za uchumi katika nchi moja huweza kuyumbisha uchumi wa Jumuiya. Tumeona pia kuwa Jumuiya itakabiliwa na changamoto ya kuhakikisha maamuzi yake yanatekelezwa. Kadri nchi zinavyokuwa nyingi ndivyo inavyokuwa vigumu zaidi kutekeleza mipango, hasa kama upande wa Sekretariati unalegalega au kama muundo uliopo hauwezi kuendana na mabadiliko yanayotokea. Changamoto kubwa, hata hivyo, itakuwa ni ushindani kutoka kwa Jumuiya nyingine na hasa kwa wale watakaopoteza maslahi yao kutokana na nchi hizi kuungana. Kama Jumuiya isipokuwa makini inaweza kuwa mhanga wa michakato ya kimataifa inayoendelea sasa. Changamoto nyingine itakayoikabili Jumuiya ni kuhakikisha kuwa inaendelea kuvutia wanachama wengi zaidi. Pamoja na kuwa ina malengo makubwa ya kufikia Shirikisho tofauti na Jumuiya nyingine, bado ni Jumuiya yenye wanachama wachache kabisa ukilinganisha na nyingine za Afrika. Hili litatokea tu kama nchi nyingine zitaona manufaa yatokanayo na Jumuiya.

Marejeo

Baregu, Mwesiga (2007). "Towards the Federation of East Africa: The Logic of Fast Tracking" A Keynote address presented at the Conference for Capacity Building for the Fast Tracking of the East African Common Market, Organized by CUTS International 29th – 30th January.

Brown, Chris (2001). *Understanding International Relations*, New York, St. Martin's Press.

Burgio, Giuseppe (2006) "Main Challenges Facing European Union" in Heikkilla, Thomas, *The Europe 2050: Challenges of the Future, Heritage of the Past*, Ministry of Foreign Affairs of Finland, Helsinki.

Daily News, Desemba 2, 2006.

EAC (2000). The Treaty for the Establishment of the East African Community.

EAC (2004). Report of the Committee on Fast Tracking East African Federation, submitted to the Sixth Summit of Heads of State of the East African Community, Arusha, 26th November.

Holthus, M. (2002). "Structural Funds and Regional Policy of the European Union Reducing Economic and Social Disparities." Discussion paper from the Proceedings of an EAC Seminar in Arusha, held on 19th-20th March 2001 whose theme was "Dialogue on Regional Integration in East Africa."

http://www.eac.int/ivdp/basin. Accessed on May 22, 2004.

http://www.unctad.org. Accessed May 2007.

IMF (2007). IMF Country Report No. 07/113. Available at http://www.imf.org.

IMF (2007). IMF Country Report No.07/138. Available at http://www.imf.org.

IMF (2007). IMF Country Report No. 07/80. Available at http://www.imf.org.

Kasaija, Phillip (2004). "Regiona. Integration: A Political Federation of the East African Countries" in *African Journal of International Affairs*, Vol. 7. Nos. 1&2, pp.21-34.

Kiflewahid, Ezana Berhane (2004). "Does East Africa Constitute an Optimal Currency Area?" An honours essay submitted to Carleton University in fulfillment of the requirements for the degree of Bachelor of Arts in Economics.

Legum, Collin (1962). Pan-Africanism: A Short Political Guide, London, The Pall Mall Press Ltd.

Liinekanen, Erkki (2004). "Innovation and Opportunities in the Enlarging Europe." Speech by Member of the European Commission Responsible for Entreprise and the Information Society, Copenhagen, 29 January.

Mattli, Walter (1999). The Logic of Regional Integration: Europe and Beyond Cambridge, Cambridge University Press.

Muthaura, Francis (2002). "The Process for the EAC Regional Integration." Discussion paper from the Proceedings of an EAC Seminar in Arusha, held on 19th-20th March 2001 whose theme was "Dialogue on Regional Integration in East Africa."

Nyanjom, O. (2005). "Can the EAC help to Deliver the Millenium Development Goals?" in Rok Ajul (ed.), The Making of a Region: The Revival of the East African Community, Institute for Gkobal Dialogue, Braamfontein.

Shams, Rasul, (2002). "Vision and Historical Development of European Integration from Customs Union to Economic and Monetary Union." Discussion paper from the Proceedings of an EAC Seminar in Arusha, held on 19th-20th March 2001 whose theme was "Dialogue on Regional Integration in East Africa."

Straubhaar, Thomas, (2002). "Theoretical Expectations on Economic Integration." Discussion paper from the Proceedings of an EAC Seminar in Arusha, held on 19th-20th March 2001 whose theme was "Dialogue on Regional Integration in East Africa."

The East African, Aprili 3, 2007.

Vayryenen, Raimo (2006). "Old and New Borders in Europe" in Heikkilla, Thomas, *The Europe 2050: Challenges of the Future, Heritage of the Past*, Ministry of Foreign Affairs of Finland, Helsinki.

Wangwe, Samuel (2002). "Proposals to Address Economic and Social Disparities in EAC." Discussion paper from the Proceedings of an EAC Seminar in Arusha, held on 19th-20th March 2001 whose theme was " Dialogue on Regional Integration in East Africa."